

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji [W])

WILAYA YA BAGAMOYO:

Simu: 023 - 2440164

Fax: 023 – 2440338

Email: ded.bagamoyo@pwani.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)

S.L.P. 59,

BAGAMOYO

MIKOA WA PWANI

Kumb.Na.HWB/A.20/75/142

17/11/2017

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA WASAIDIZI WA HESABU

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kuomba nafasi ya Ajira kwa masharti ya Mkataba kwa nafasi tajwa hapo chini kwa kuzingatia masharti ya waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.14 wa mwaka 2002 unaohusu miundo ya Utumishi wa kada zilizochini ya Wizara ya Fedha unaohusu miundo ya kada za Wasaidizi wa Hesabu chini ya Ofisi ya Rais. Kwa kuzingatia Kibali cha Ajira za wasaidizi wa Hesabu chenye **Kumb.Na.AH.161/164/02** cha tarehe **24/10/2017** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

1. NAFASI YA KAZI: MSAIDIZI WA HESABU

-Nafasi 2

2. KAZI NA MAJUKUMU

- Kuandika na kutunza "Register"zinazohusu shughuli za uhasibu.
- Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha.
- Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki.
- Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, Hesabu za Benki na Amana.
- Kutunza Majalada yenye kumbukumbu za hesabu.

3. SIFA ZA KUAJIRIWA

Kuajiriwa wenye Cheti cha ufaulu cha Kidato cha IV, Cheti cha ATEC Level II au "Foundation Level" kinachotolewa na NBAA.

4. MSHAHARA

TGS B1 kwa mwezi

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO NI LAZIMA KUZINGATIWA

1. Mwombaji ni lazima awe ni Raia wa Tanzania.
2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai
3. Awe hajawahi kupunguzwa/kufukuzwa kazi Serikalini.
4. Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu elimu ya Sekondari ("Result Slip" hazikubaliki) na vyuo vya mafunzo/taaluma.
5. Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni.
6. Maombi ni lazima yaambatanishwe na wasifu (Curriculum Vitae) zenye mawasiliano ya uhakika Anuani, Barua pepe na namba ya simu.
7. Awe na umri wa zaidi ya miaka 18 na usiozidi miaka 45.
8. Mwombaji awe hajawahi kuajiriwa Serikalini na kupata cheki namba.
9. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya Nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE)

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA NI TAREHE 01/12/2017 SAA 9:30 ALASIRI PIA MAOMBI YOTE YATUMWE KWA NJIA YA POSTA KUPITIA ANUANI HAPO CHINI NA SI VINGINEVYO.

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO,
S.L.P. 59,
BAGAMOYO

**TANGAZO HILI PIA LINAPATIKANA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI
www.bagamoyodc.go.tz**

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-

Eng. Kayilla J.M.
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BAGAMOYO

Nakala: Watendaji wa Kata,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 59,
BAGAMOYO

“ “ Mbao za Matangazo zote,
Halmashauri ya Wilaya,
BAGAMOYO